NMB
Karibu yako

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 25 wa mwaka wa wanahisa wa Benki ya NMB utafanyika kwa njia ya mtandao siku ya Alhamisi tarehe 5 Juni, 2025 kuanzia saa 4 asubuhi.**

**Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

25.1 MATANGAZO NA AKIDI
25.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
25.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 24 ULIOFANYIKA TAREHE 7 JUNI 2024
25.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 24 WA WANAHISA
25.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2024
25.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2024
25.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA VIWANGO VYA MALIPO YA WAKURUGENZI
25.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI
25.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2025
25.10 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MABADILIKO KATIKA KATIBA YA KAMPUNI.
25.11 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria Mkutano lazima wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au Taarifa ya Akaunti (CSDR Account Statement).
2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya Benki ya NMB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe **Consolatha.Resto@nmbbank.co.tz** kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Jumatano tarehe 4 Juni 2025.
3. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria kikao watahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za uwakilishi (proxy forms) zitapatikana kwenye tovuti ya Benki ya NMB (**www.nmbbank.co.tz**).
4. Wakurugenzi wamependekeza malipo ya gawio la shilingi 428.85 kwa kila hisa, ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 214.4 kutokana na faida baada ya kodi ya mwaka 2024 ya shilingi bilioni 643.

**Tarehe za kuzingatia:**

- Tarehe ya tangazo: - 14 Mei 2025
- Hisa kuuzwa pamoja na gawio: - 14 Mei 2025
- Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio: - 02 Juni 2025
- Hisa kuanza kuuzwa bila gawio: - 03 Juni 2025 na kuendelea
- Daftari la wanahisa kufungwa: - 05 Juni 2025
- Malipo ya gawio kwa wanahisa: - 19 Juni 2025

Kwa agizo la Bodi.

Consolatha R. Mosha
**Kaimu Katibu wa Kampuni**
14 Mei 2025